بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيم

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

**UMOJA WA SHULE ZA KIJESHI**

**MTIHANI WA MAANDALIZI KABLA YA MTIHANI WA TAIFA**

**KIDATO CHA NNE**

**015 ELIMU YA DINI YA KISLAMU**

**MUDA:Masaa 3:00** **06 AGOSTI 2026**

---

## MAELEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C , zenye jumla ya maswali kumi na moja.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali mawili (2) kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama kumi na sita (16), sehemu B ina alama hamsini na nne (54) na sehemu C ina alama thelathini (30).
4. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

**SEHEMU A**: (Alama 16).

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika kijitabu Chako cha kujibia .

i. Bainisha sura inayowafunza waislamu adabu ya kuomba dua katika sura zifuatazo :
A: Suratul Falaq B: Suratul Fat-hat C: Suratul Ikhlas D: Suratul Nasri E: Suratul Lahab.

ii. Katika swala ya maiti, takbira ya nne watu husema nini?
A: Husoma Suratul-fatha. B: Kumuombea dua maiti. C: Kumswalia Mtume (S.A.W).
D: Kumuombea dua maiti pamoja na waislamu wote. E: Kuzidisha dua ili maiti asamehewe madhambi yake.

iii. Elimu yenye manufaa kwa mujibu wa Qur-an huwa na sifa ipi ?
A: Inatoa ujuzi na maarifa. B: Hufundisha elimu ya dunia na akhera. C: Inamuezesha mtu kufanya ibada D: Hupelekea mtu kupata ajira. E: Humpelekea mtu kupata riziki ya halali.

iv. Kwa nini Uislamu ndio dini sahihi inayostahiki kufuatwa na kila mwanaadamu?
A: Ni dini iliyokuja mwisho wa karne ya sita. B: Ni dini inayomtaka mtu kutafuta elimu.

C: Ni dini inayomfanya mtu kufanya ibada. D: Ni dini ya Allah (sw) aliyemuumba mwanaadamu kwa lengo. E: Ni dini inayoongozwa na mtume wa mwisho.

v. Wadda, Yaghuutha, Yauuka, Nasra na Suwa'a, waliabudiwa na kaumu gani ya Nabii ?
A: Ibrahim (as) B: Nuhu (as) C: Muhammad (saw) D: Mussa (as) E: Idrissa (as).

vi. Katika elimu ya hadithi neno 'Al-Jarhi' hutumika kuonesha msimulizi wa hadithi mwenye sifa gani?
A: Nzuri B: Ucha mungu C: Mkweli D: Mbaya E: Hafifu

vii. Miongoni mwa mafunzo yatokanayo na maandalizi ya kii-lham ya Mtume (saw) ni pamoja na:-
A: Hatuna budi kuwaandaa watoto wetu kuwa makhalifa wa Allah (sw) hapa duniani.
B: Utekelezeji wa ujumla wa Qur-ani ni kazi nzito na yenye misukosuko.
C: Maingiliano ya mataifa na kibiashara ni katika neema za Allah (sw).
D: Kutafuta elimu ni jambo muhimu sana.
E: Nusura na mafanikio hutoka kwa Allah (sw)

viii. Ni kwa namna gani uislamu humuezesha muumini kuwa katika ibada muda wote wa maisha yake?
A: Humlazimisha kutekeleza nguzo tano za dini. B: Katika uislamu kuna nguzo sita za imani.

C: Uislamu umeondoa uhuru wa watu kupumzika. D: Kuna majengo ya ibada za waislamu kote duniani.
E: Ibada inahusu kila jambo analoridhia Allah (sw).

ix. Ni sababu gani ya vitabu vilivyotangulia vya Allah (sw) kutajwa ndani ya Qur-ani?
A: Vimetajwa ili kuwafahamisha waislamu juu ya uwiano, usahihi na upotofu wa mafundisho hayo na usahihi uliomo katika Qur-ani.
B: Vimetajwa ili watu wachague kitabu kipi wafuate kwa mujibu wa maisha yao.
C: Vimetajwa ili kuwakumbusha watu kuwa kuna mitume iliyopewa vitabu hivyo.
D: Vimetajwa ili kuondoa dhana ya watu kuwa Allah (sw) ameteremsha Qur-an pekee.
E: Vimetajwa ili kuwawezesha watu wa zama zilizopita kupata muongozo wao.

x. Misingi mikuu mitatu ya Fig-hi ni
A: Qur-an, Ijmaa, na Sheria. B: Qur-an, Sunna, na Ijtihaad. C: Sheria, Qiyas, na Ijmaa.
D: Taadil, Qur-an na Ijitihaad. E: Sunna, Hadithi, na Jarah.

2. Oainisha maana ya swala za sunna zilizopo katika orodha ‘A’ na aina za swala hizo katika orodha ‘B’. kisha andika herufi ya jibu sahihi kwa kila kipengele katika kijitabu chako cha kujibia

| **ORODHA A** | **ORODHA B** |
|---|---|
| i. Huswaliwa rakaa 1,3,5,7 na zaidi katika Thuluthi ya mwisho wa usiku mara tu baada ya swala ya Isha. | A. Swalatul- Tawbah |
| ii. Huswaliwa kila siku baada ya jua kupanda Kiasi cha mita tatu jua kuchomoza na kabla Ya adhuhuri. | B. Swalatul Istikhaara. |
| iii. Huswaliwa rakaa mbili muda wowote kwa ajili ya kutubia baada ya muislamu kufanya kosa. | C. Swalatul witri. |
| iv. Ni swala ya rakaa mbili kwa ajili kuomba Mvua baada ya dhiki na ukame. | D. Swalatul Istisqaai. |
| v. Ni swala ya rakaa mbili muda wowote kwa ajili ya kuomba msaada au utatuzi wa tatizo Lililotokezea. | E. Swalatul Tahajjud. |
| vi. Ni swala inayoswaliwa muda wowote kwa ajili kuomba msaada na muongozo kwa Allah (sw) juu ya uamuzi wa jambo lolote zuri. | F. Swalatul haja |
| | G. Swalatul dhuha |
| | H. Swalatul Iftisqai |

**SEHEMU B:** (Alama 54)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

3. Qur-an tukufu imesimulia matukio mbali mbali ambayo yanathibitisha kuwepo kwa Allah (S.W) kupitia historia ya maisha ya mwanadamu. Tumia matukio sita (6) kuthibitisha kauli hii.

4. Mafundisho ya uislamu yana mjali kila mtu na kumpatia haki zake zote za msingi. Elezea hoja sita (6) kwa kutumia mtumwa katika dola ya kiislamu.

5. Jamii ya sasa kuna baadhi ya watu hutenda mengi bila kujua hili ni kosa la aina gani. Ukiwa ni mtaalamu uliechaguliwa wafahamishe watu kwa kutumia aina tatu (3) za makosa na kila kosa litolee mfano mmoja.

6. Umeteuliwa katika kijiji unachoishi kutoa darasa maalum la mirathi katika kipengele cha umuhimu. Tumia hoja sita (6) kuwafahamisha juu ya dondoo hiyo.

7. Elezea mafunzo sita (6) yatokanayo na Hijja ya kuaga ya Mtume Muhammad (S.A.W) kwa jamii ya waislamu wa leo.

8. Baada ya kufa Mtume (S.A.W) dola ya kiislamu iliongozwa na swahaba Abubakar (R.A) na wakati huo kuna baadhi ya watu waliritadi (uasi). Jadili sababu zilizopelekea uasi au kuritadi mara tu ya kufa Mtume (S.A.W).

**SEHEMU C:** (Alama 30)

9. Fafanua njia nne (4) kwa namna gani waislamu watakiendea kitabu (Qur-an) cha Allah (S.W) katika maisha yetu.

10. Elezea hoja nne (4) za msingi zilizohitajika kuwepo uandishi wa hadithi wakati wa maswahaba.

11. Mzazi wako mara hii amerudi kufanya ibada ya Hijja na alikuelezea faida mbali mbali alizozipata wakati akitekeleza ibada hiyo. Wafahamishe wenzako kwa kuwapa nukta sita (6) ambazo mzazi wako alikufafanulia.

**Wabillahi Tawfiiq**